Sudan Kusini

Kitabu cha mwanafunzi

# Kiswahili 1

**Kiswahili kwa kidato cha kwanza (1)** kimeandikwa na wizara ya Elimu na Mafunzo kwa jumla, Ikishirikiana na wataalam wa lugha.

Kitabu hiki kinamwelimisha mwanafunzi kwa mazoezi na vitendo.

**Kila darasa linajumuisha Kitabu cha Mwanafunzi na Mwongozo wa Mwalimu..**

**Kila Kitabu cha mwanafunzi kinakupa:**

- ufafanuzi mwafaka wa mtaala wa kitaifa
- Msingi bora katika kiswahili.
- Uwasilishaji na ufafanuzi wa hoja unazotakiwa kujifunza.
- Mazoezi mwafaka yanayoonyesha jinsi Kiswahili Kinaweza kutumika katika mifano halisi maishani.
- Fursa ya ushirikiano kupitia kwa kazi ya vikundi.
- Michoro ya kusisimua.

**Masomo yote katika mfululizo huu wa msingi yalitengenezwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Mkuu, Jamhuri ya Sudan Kusini.**

**Vitabu vimeundwa kutekeleza somo la shule za msingi,na wakati huo huo kuwawezesha wanafunzi na ujuzi unaofaa katika jamii ya kisasa ya kimataifa**

**Kitabu hiki ni Mali ya Wizara ya Elimu na Mafunzo.**

**Kitabu hiki hakiruhusiwi kuuzwa.**

**Kitabu kitakachopatikana kikiuzwa kwa njia yoyote kitatawaliwa na muuzaji kuchukuliwa hatua za kisheria.**

**Funded by:**

GLOBAL PARTNERSHIP for EDUCATION
quality education for all children

Sudan Kusini

THE REPUBLIC OF SOUTH SUDAN
MINISTRY OF GENERAL EDUCATION AND INSTRUCTION

Kitabu cha mwanafunzi

# Kiswahili 1

## Kidato cha Kwanza



**Kitabu hiki ni Mali ya Wizara ya Elimu na Mafunzo.**

**Kitabu hiki hakiruhusiwi kuuzwa.**

**Kimetadhiliwa na:**

GLOBAL PARTNERSHIP for EDUCATION
quality education for all children

# Jinsi ya kutunza kitabu chako.

**Mambo muhimu ya kuzingatia**

1. Unaombwa kuhakikisha umenawa mikono kabla ya kukitumia kitabu chako.
2. Tumia kalamu ya rangi kuonyesha kazi iliyofanywa.Usikunje karatasi za vitabu.
3. Kitabu kikiharibika,hakikisha kinakarabatiwa kwa haraka.
4. Kuwa mwangalifu wakati unapomwazimu mwenzako kitabu.
5. Tafadhali kiweke kitabu chako mahali pakavu na pasipokuwa na unyevu.
6. Unapokipoteza kitabu chako, mjulishe mwalimu wako.

**Mambo unayokatazwa kufanya.**

1. Usiandike ndani au juu ya kitabu chako.
2. Usikate michoro iliyokitabuni.
3. Usirarue kurasa zozote kitabuni.
4. Usikiache kitabu kikiwa kimefunguliwa.
5. Usikiweke kitabu chako kwenye mkoba uliojazwa vitabu zaidi.
6. Usikitumie kitabu chako kujifunika wakati wa mvua.
7. Usikikalie kitabu chako.

Sudan Kusini

KIDATO CHA
1

# Kiswahili

*Kitabu cha Mwanafunzi*

© 2018, THE REPUBLIC OF SOUTH SUDAN, MINISTRY OF GENERAL EDUCATION AND INSTRUCTION.
All rights reserved. No part of this book may be reproduced by any means graphic, electronic, mechanical, photocopying, taping, storage and retrieval system without prior written permission of the Copyright Holder. Pictures, illustrations and links to third party websites are provided in good faith, for information and education purposes only

Ilifadhiliwa na:

Kitabu hiki ni Mali ya Wizara
Kimetadhiliwa na: ya Elimu na Mafunzo.

GLOBAL PARTNERSHIP for EDUCATION
quality education for all children

**KITABU HIKI HAKIRUHUSIWI KUUZWA.**


FOREWORD

I am delighted to present to you this textbook, which is developed by the Ministry of General Education and Instruction based on the new South Sudan National Curriculum. The National Curriculum is a learner-centered curriculum that aims to meet the needs and aspirations of the new nation. In particular, it aims to develop (a) Good citizens; (b) successful lifelong learners; (c) creative, active and productive individuals; and (d) Environmentally responsible members of our society. This textbook, like many others, has been designed to contribute to achievement of these noble aims. It has been revised thoroughly by our Subject Panels, is deemed to be fit for the purpose and has been recommended to me for approval. Therefore, I hereby grant my approval. This textbook shall be used to facilitate learning for learners in all schools of the Republic of South Sudan, except international schools, with effect from 4th February, 2019.

I am deeply grateful to the staff of the Ministry of General Education and Instruction, especially Mr Michael Lopuke Lotyam Longolio, the Undersecretary of the Ministry, the staff of the Curriculum Development Centre, under the supervision of Mr Omot Okony Olok, the Director General for Quality Assurance and Standards, the Subject Panelists, the Curriculum Foundation (UK), under the able leadership of Dr Brian Male, for providing professional guidance throughout the process of the development of National Curriculum and school textbooks for the Republic of South Sudan since 2013. I wish to thank UNICEF South Sudan for managing the project funded by the Global Partnership in Education so well and funding the development of the National Curriculum and the new textbooks. I am equally grateful for the support provided by Mr Tony Calderbank, the former Country Director of the British Council, South Sudan; Sir Richard Arden, Senior Education Advisor of DfID, South Sudan. I thank Longhorn and Mountain Top publishers in Kenya for working closely with the Ministry, the Subject Panels, UNICEF and the Curriculum Foundation UK to write the new textbooks. Finally, I thank the former Ministers of Education, Hon. Joseph Ukel Abango and Hon. Dr John Gai Nyuot Yoh, for supporting me, in my previous role as the Undersecretary of the Ministry, to lead the Technical Committee to develop and complete the consultations on the new National Curriculum Framework by 29 November 2013.

The Ministry of General Education and Instruction, Republic of South Sudan, is most grateful to all these key stakeholders for their overwhelming support to the design and development of this historic South Sudan National Curriculum. This historic reform in South Sudan's education system is intended to benefit the people of South Sudan, especially the children and youth and the future generations. It shall enhance the quality of education in the country to promote peace, justice, liberty and prosperity for all. I urge all Teachers to put this textbook to good use.

May God bless South Sudan. May He help our Teachers to inspire, educate and transform the lives of all the children and youth of South Sudan.



Deng Deng Hoc Yai, (Hon.)
**Minister of General Education and Instruction, Republic of South Sudan**

# YALIYOMO

MAAMKUZI ........................................................ 1

SHULE YETU ...................................................... 22

UCHUKUZI......................................................... 41

MWILI NA USAFI ............................................... 54

NYUMBANI KWETU.......................................... 64

USHIRIKIANO, AMANI NA UTULIVU ............ 76

# SURA YA 1

# MAAMKUZI


## Mada Ndogo ya 1: Kusikiliza na kuzungumza

### Maamkuzi

**Maamkuzi** ni salamu za adabu zinazotumiwa kwa mazungumzo ya kila siku. Maamkuzi hutegemea mazingira, hali, umri, mahusiano, mila na utamaduni wa watu. Maamkuzi hutumia lugha ya heshima.

### Zoezi

**Mkiwa katika makundi ya wawili wawili, jadilianeni mchoro ufuatao.**



1. Hamjambo wanafunzi? Hatujambo mwalimu.



2. U hali gani, Wani? Salama,Deng.



3. Habari yako Okot? Nzuri, Ayen.



4. Shikamoo Mwalimu. Marahaba Lado.



5. Shikamoo baba. Marahaba mwanangu.



6. Habari jirani? Njema.



7. Habari yako kaka? Nzuri dada.

**Soma maamkuzi na miitiko yake.**

a) Habari?– Nzuri!
b) Shikamoo?– Marahaba!
c) Hujambo?– Sijambo!
d) Umeamkaje? – Nimeamka vyema!
e) Umeshindaje?– Nimeshinda vyema!
f) Salam aleikum? - Aleikum Salam!
g) Masalkheri! - Alheri/Masannuri (Asubuhi)
h) Sabalkheri! – Alheri/Sabahannuri!

## Maneno ya adabu na miitiko yake

a) Hodi? – Karibu!
b) Hodi tena? – Karibu ndani!
c) Karibu kiti ukae! - Starehe asante!
d) Pole kwa ugonjwa! - Asante nishapoa!

## Zoezi

**Igizeni maamkuzi yafuatayo kati ya viranja.**
**Mazungumzo: Shuleni**

| | |
|---|---|
| **WANI:** | **Masalkheri** Mariam? |
| **MARIAM:** | **Alheri** Wani. **Shikamoo**? |
| **JUMA:** | **Marahaba** mwenzangu. **Habari za asubuhi?** |
| **MIRIAM:** | **Njema** kabisa Kiranja mkuu.**Tafadhali** Wani, unaweza **kunisaidia** na kalamu? |
| **JUMA:** | Ndiyo ninaweza, shika**.** |
| **MARIAM:** | **Asante**. Je, nikuletee kiti? |
| **JUMA:** | **La, asante.** Ninaenda darasani. |

## 2. Alfabeti ya Kiswahili

**Irabu:**

**Irabu** pia huitwa **vokali.** Tunapotamka irabu, kinywa huwa wazi na hewa hutoka mapafuni na kuto nje ya kinywa bila kuiwa na ala yoyote ya kutamkia. Irabu za Kiswahili ni tano. Nazo ni:

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **a** | **e** | **i** | **o** | **u** |

## Konsonanti za Kiswahili

Soma konsonanti za Kiswahili zifuatazo.

**b, ch, d, dh, f, g, gh, h, j, k, kh l, m, n, ng', ny, p, r, s, sh, t, th, v, vy w, y, z**

Konsonanti za Kiswahili huainishwa kwa kuzingatia namna/jinsi zinavyotamkwa na mahali zinapotamkiwa. Kiswahili kina aina za konsonanti zifuatazo:

a) vipasuo/vizuiwa
b) vikwamizwa
c) nazali
d) vizuiwa kwamizwa
e) kitambaza
f) kimadende
g) viyeyusho/nusu irabu

## Tazama na usome jedwali lifuatalo.

| Aina ya konsonati | midomo | Mido na meno | meno | Ufizi | Kaakaa gumu | Kaakaa laini | Glota/ korome |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Vipasuo/vuiwa | p, b | | | t, d | | | |
| Vikwamizwa | | f<br>v | th<br>dh | s sh<br>z | | kh<br>gh | h |
| Nazali/ving'ong'o | m | | | n | ny | ng' | |
| Vizuiwa kwamizwa | | | | | ch<br>j | | |
| kitambaza | | | | l | | | |
| kimadende | | | | r | | | |
| kiyeyusho | w | | | | y | | |

Lugha ya Kiswahili haina silabi **X** na**Q** maana hakuna maneno ya Kiswahili yanayoandikwa kwa silabi **X au Q.**

Katika kuunda maneno ya Kiswahili, unachukua herufi ya irabu na konsonanti unaweka pamoja. Kwa mfano:

**mw+a+n+a+f+u+nz+i=mwanafunzi.**

**d+a+r+a+s+a=darasa.**

**Tofauti ya irabu na konsonanti ya kiswahili**

Tofauti ya irabu na konsonanti za kiswahili ni kwamba:

1. Irabu ni tano tu lakini konsonanti ni nyingi, (26).
2. Unapohesabu konsonanti, hupaswi kutaja. Kwa mfano, tunaanza kwa **b mpaka z** bila kutaja irabu yoyote ya Kiswahili.
3. Unapotamka irabu, unafaa kujua ala za kutamkia hazikutani ila ncha ya ulimi ndiyo husonga mbele, nyuma au kuinuka juu kwa paa la kinywa.


## Zoezi

1. Andika irabu za Kiswahili kwa mpangilio.
2. Andika konsonanti za Kiswahili kwa mfuatano sahihi.
   s, th, b, d, f, gh, p, h, j, g, ch, k, m, v, n, ng', ny, r, l, sh, t, w, y, z, dh.
3. Jaza irabu iliyoachwa:
   __________, e, _________, _________ u.

**Mada Ndogo ya 2:** **Kusoma**

## I. MAWASILIANO YA ADABU KATIKA FAMILIA

**Katika makundi ya wawili wawili, jadilianeni mchoro ufuatao, na umsomee mwenzako kifungu hiki.**



Naikumbuka siku hiyo, mamangu alipoamka asubuhi alitupikia chai. Alimwamsha dadangu mdogo na kumtuma amwite kaka. Baba

alifika na kutuamkua, “Hamjambo wanangu?’’Nasi tukamjibu, “Hatujambo baba.”

Siku hiyo ilikuwa ya ukumbusho wa babu yetu ambaye aliaga dunia miaka miwili iliyopita. Marehemu babu alikuwa mtu wa vichekesho mpaka siku yake ya mwisho. Siku hiyo aliniita na kunipa mkono wa buriani. Sikuelewa alichomaanisha mpaka nilipoelezwa baadaye. Nililia sana nilipompoteza babu yangu. Marafiki wangu walifika kunipa pole.

Shangazi alifika akiwa na wageni. Nyuma yao kulikuwa na vijana. Nilijua hao ni binamu. Tulikimbilia kuwapokea na kuwakaribisha nyumbani. Kila mmoja alikuwa amebeba mzigo. Si vikapu si magunia si kuku si mikungu ya ndizi.

“Shangazi, poleni kwa safari!” Kaka yangu aliwaamkua.

“Tumepoa!” Shangazi alijibu.

Mara ami alituita akiwa na amu huku amu akiwa ameshika kamba ya ng’ombe. Alinipa nimpelekee mkoi. Bila shaka tulijua kuwa walikuwa wanataka kuchinja ng’ombe. Niliipeleka haraka na kurudi. Kabla sijafika karibu na nyumba ya ami, nilisikia, “Mkota, njoo hapa.” Sauti ilitoka sebuleni. Kumbe alikuwa mjomba na mkazajomba.

“Hujambo mpwa?” Aliniamkua.

“Sijambo mjomba na mkazamjomba! Wapi Abineri?” Niliuza.

Shughuli zilikuwa nyingi kama za kumbikumbi msimu wa vuli. Mara wajukuu wote tuliitwa tupange na kupangusa viti. Kwa kweli sitaisahau siku hiyo.

## a) Zoezi:

1. Baba alipowaamkua watoto wake walimjibuje?
2. Kwa nini siku hiyo ilikuwa ya muhimu?
3. Sababu ya msimulizi kulia ilikuwa ni nini?
4. Mke wa mjomba anaitwaje?
5. Ami na amu ni akina nani?

## b) Mkiwa kwa makundi ya wawili wawili,igizeni maamkuzi baina ya Wani na babu yake.

**Mazungumzo: Nyumbani**

**Wani:** **Hodi?**
**Babu:** **Karibu!**
**Wani:** **Hodi tena?**
**Babu:** **Karibu ndani! Karibu kiti ukae!**
**Wani:** **Starehe asante!**
**Babu**: **Hujambo** mjukuu wangu?
**Wani:** **Sijambo** babu. S**hikamoo**?
**Babu:** Marahaba, **habari za nyumbani** kwenu?
**Wani:** **Njema** babu. Nimeona nije **nikujulie hali**. Je, nyanya **hajambo**?
**Babu:** **Hajambo!** Ameenda kwa jirani aliyefiwa **kumpa makiwa**.
**Wani**: Oo! Ukimwona jirani mwambie **pole** sana. Jirani aliachwa na nani?
**Babu:** **Asante,** nitamwambia. Ameachwa na mume wake.

**c) Salamu zifuatazo hujibiwaje?**

1. Shikamoo?
2. Hujambo?
3. Mama hujambo?
4. Wani alikuwa ameenda kwa babu kufanya nini?
5. Maneno **kuachwa na mume** yanamaanisha nini?

**d) Chagua maneno ya adabu na heshima katika swali (b) hapo juu.**


**e) Tunga sentensi ukitumia maneno yafuatayo.**


1. samahani
2. kunradhi
3. safiri salama
4. siku njema
5. kila la heri
6. kwaheri ya kuonana

## II. Sehemu za nyumbani

**Ufahamu**

**Soma kifungu kifuatacho.**

| | |
|---|---|
|  |  |

Waswahili husema nyumbani ni nyumbani. Kuwe shambani ni nyumbani. Kuwe mjini ni nyumbani. Watu wanaoishi mashambani hufurahia hewa na mazingira safi. Mito hutiririka maji safi. Misitu mingi huisafisha hewa na kuvuta mvua. Hii ndiyo hufanya watu wa mashambani kuwa wachangamfu kila wakati. Nyumba zao huwa si kubwa kama za mijini.

Nyumba nyingi za mijini zimejengwa kwa mawe. Watu wa mijini huziita nyumbausi. Nyumba hizi huwa na vyumba vingi. Sebuleni ni chumba cha kupokea wageni. Wageni wakifika hukaribishwa kwa furaha na kukalia makochi.

Baada ya kupumzika, wageni hukaribishwa katika chumba cha maakuli. Baada ya kula, mgeni anaweza kuhisi haja ndogo au kubwa. Hapo, mgeni huonyeshwa msalani. Msalani huwa kuna vyumba viwili. Kuna bafu na choo. Bafu ni pa kuoga ili kupunguza joto na kutoa jasho baada ya shughuli nyingi za mchana. Choo nacho ni cha kutimizia haja.

Baada ya chakula cha jioni, mgeni hupelekwa katika chumba cha malazi. Huko, yeye huonyeshwa kitanda chenye godoro, mashuka na mablanketi yenye sufi nzuri na marashi ya kuvutia. Ndara huwa chini ya kitanda ili asikanyage chini na kuvaa akienda msalani. Kwa ukuta karibu na kitanda, huwa na swichi ya stima ili kuzima taa kabla ya kuingia kitandani. Katika chumba hiki, wakati mwingine, unaweza kupata meza ndogo ya kuwekea msaafu ama msumaa au kandili.

Asubuhi ya siku inayofuata, jikoni huwa kuna shughuli nyingi kama za mzingani. Huko ndiko mapishi hutendekea na kukaribisha siku mpya.

## Maswali

1. Chumba cha kupumzikia huitwaje?
2. Panka huwa wapi katika chumba?
3. Taja tofauti mbili za mazingira ya mjini na mashambani.
4. Taja vitu vitatu vinavyopatikana katika chumba cha kulala.
5. Tumia msamiatai ufuatao kutunga sentensi.
    i. nyumbausi
    ii. feni
    iii. video
    iv. sakafu
    v. msalani

## Mada Ndogo ya 3: Sarufi

## Aina ya maneno

1. **Nomino** ni majina ya watu,mahali,vitu, milima, wanyama na ndege.Kwa mfano:
    a) Watu - Juma,Abdalla, Salima.
    b) Mahali - Kenya,Sudan Kusini,mto,mlima.
    c) Vitu - meza,kabati,gari,kioo.

d) Wanyama - ndovu,fisi,mamba.
e) Ndege - tausi,bundi, kuku.
f) Milima-Mlima Kenya,Mlima Kinyeti

*Mfano katika sentensi:*
**Jirani** alinitembelea. – **Jirani** ni nomino.

2. **Kitenzi** ni neno linaloonyesha kitendo anachofanya mtu,mnyama au kitu.

*Mifano ya vitenzi:*kimbia,lala,kula,lima,iga,ficha,soma naenda.
*Mfano:*Mtoto **analala.** –Neno **analala** ni kitenzi.

3. **Kiwakilishi** ni neno ambalo linatumika badala ya kutaja nomino. Huchukua nafasi ya nomino.Mifano ya viwakilishi ni:

| **umoja** | **wingi** |
|---|---|
| mimi | sisi |
| wewe | nyinyi |
| yeye | wao |

*Mfano katika sentensi:***Mimi** ninasoma. Neno **mimi** ni kiwakilishi.

4. **Kivumishi** ni neno linalotoa sifa za nomino. Huongea juu ya sifa za nomino inayohusika. Hutumika baada ya nomino au kiwakilishi. *Mfano:*-zuri,-baya,-ema,-angu,-ake, -eusi na kadhalika.

*Mfano katika sentensi:*
Mwanafunzi **mtukutu** ametoroka. Neno **mtukutu**ni kivumishi.

5. **Kielezi** ni neno linaloelezea jinsi kitendo kilivyotendeka,kitatendeka au kinatendeka.Mfano: wepesi,haraka,mno,vibaya,vizuri na kadhalika.

***Mfano:***

Mwalimu anafunza **vizuri**. Neno **vizuri** ni kielezi.

6. **Vihisishi** ni maneno yanayodhihirisha hisia. Hisia hizo ni kama mshangao, uchungu, huruma, furaha na madharau. Mifano katika sentensi:
   a)**Maskini!** Mtoto ataanguka. (Huruma)
   b)**Huraah!** Timu yetu imeshinda. (Furaha)
   c)**Lo!** Leo Yosif amechelewa. (Mshangao)

7. Viunganishi ni maneno yanayounganisha neno na neno au sentensi na sentensi. Mifano: na, mithili ya, mfano wa, kana kwamba, pamoja na, fauka ya na au. Mfano katika sentensi:
   a) Juma **na** Mariam (nomino na nomino)

   b) Rehema anafua **ilhali** Juma anafyeka nyasi. (kifungu kimoja na kingine)

8. Vihusishi ni maneno yanayodhihirisha uhusiano kati ya nomino na nyingine. Kwa mfano: kando ya, juu ya, karibu na, mbele ya na nyuma ya. Mfano katika sentensi:
   a) Mariam anatembea **kando ya** Juma.
   b) Ubao uko **mbele ya** darasa.

## Zoezi

**a) Taja vitenzi vilivyotumika katika sentensi zifuatazo:**

1. Kaka amerudi.
2. Yeye alimshukuru sana.
3. Baba alitusalimia.
4. Simba alimkimbiza mama.
5. Salamu za rafiki yangu zilinifurahisha.
6. Maji yalimumwangikia babu.

**b) Pigia mstari nomino katika aya hii.**

Nilipoamka jana, nilimwita dada ili tunywe uji.Mama alitoka jikoni akibeba vikombe, mkatena siagi.Baba alifika na kuombea kiamsha kinywa.

**c) Tunga sentensi ukitumia:**

1. Kiwakilishi
2. Nomino
3. Kitenzi
4. Kivumishi
5. Kielezi
6. Kihusishi
7. Kihisishi
8. Kiunganishi

**d) Maneno yaliyopigiwa mstari ni ya aina gani? Eleza sababu ya kulichagua jibu lako.**

Jioni hiyo, kaka alirudi nyumbani huku amebeba mkungu wa ndizi. Sote tulimwangalia kwa furaha kwani alikuwa mkulima mwenye bidii. Hakuzoea kukaa barazani huku simu mkononi kama vijana wa siku hizi. Alijua fika kuwa jamii lazima ipate chakula. Aliuweka chini, alimwita wifi amletee kisu. Alikata chane za ndizi nakuzipanga. Zote zilikuwa kumi na nane. Alinipa chane tatu nimpelekee nyanya. Alimwita mnuna wangu akampa nne na kumwambia ampelekee mama. Wifi alipewa tatu. Mkoi alipewa tatu ampeleke kwa amu na binamu naye akapewa zilizobaki apeleke kwa ami. Tangu siku hiyo, nilijifunza kuwa kiongozi kutoka kwa kaka.

## Mada Ndogo ya 4: Kuandika

## I. Upatanisho wa kisarufi

Katika Kiswahili, sentensi huchukua viambishi vya upatanisho wa kisarufi. Viambishi vya upatanisho wa kisarufi ndivyo hudhihirisha ngeli ya nomino husika. Kila nomino iko katika kundi lake. Makundi haya ya nomino ndiyo ngeli za nomino. Kwa mfano, nomino mtoto iko katika ngeli ya **A-WA**. Yaani kiambishi **a-** katika umoja na **wa-**

katika wingi. Viambishi ngeli hivi huambatishwa kwenye kitenzi kama ilivyo kwenye jedwali lifuatalo.

## Tazama na usome jedwali ngeli.

| | | Ngeli | Umoja | Wingi | Sentensi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | | **A**<br>**WA** | mtoto | watoto | Mtoto mzuri **a**nacheza.<br>Watoto wazuri **wa**nacheza. |
| 2. | | **U**<br>**I** | mche | miche | Mche mkubwa **u**tapaliliwa.<br>Miche mikubwa **i**tapaliliwa. |
| | | **KI**<br>**VI** | kiti | viti | **Ki**ti cha mgeni **ki**mevunjika.<br>**Vi**ti vya wageni **vi**mevunjika. |
| 4. | | **LI**<br>**YA** | dawati | madawati | Dawati **la**ke **li**menunuliwa.<br>Madawati **ya**o **ya**menunuliwa. |
| 5. | | **I**<br>**ZI** | penseli | penseli | Penseli ndogo **i**mepotea.<br>Penseli ndogo **zi**mepotea. |
| 6. | | **U**<br>**ZI** | ukuta | kuta | Ukuta mpya **u**najengw**a**.<br>Kuta mpya zinajengwa. |
| 7. | | **U**<br>**YA** | ugonjwa | magonjwa | Ugonjwa mpya **u**natisha.<br>Magonjwa mapya **ya**natisha. |
| 8. | | **YA**<br>**YA** | maji | maji | Maji safi **ya**nanywewa.<br>Maji safi **ya**nanywewa. |
| 9. | | **KU** | kucheza | kucheza | Kucheza kwake **ku**navutia.<br>Kucheza kwao**ku**navutia. |
| 10. | | **U**<br>**U** | uyoga | uyoga | Uyoga **u**limea vizuri.<br>Uyoga **u**limea vizuri. |
| 11. | | **PA** | mahali | mahali | Mahali h**apa** **pa**napendeza. |
| 12. | | **MU** | mahali | mahali | Mahali humu **m**napendeza. |
| 13. | | **KU** | mahali | mahali | Mahali kule **ku**napendeza. |

## Zoezi

### a) Andika nomino hizi katika wingi.

1. mkono
2. mjukuu
3. mjomba
4. darasani
5. marashi
6. mgomba
7. jembe
8. ubua
9. unga
10. kalamu

### b) Andika sentensi hizi katika wingi.

1. Babu amefika na kigoda mkononi.
2. Mwalimu amebeba kitabu kizuri.
3. Mkulima atakuwa na jembe akienda shambani.
4. Mvua ikinyesha usicheze uwanjani.
5. Mahali pangu ni pazuri kushinda kwako.

### c) Andika sentensi hizi katika umoja.

1. Mijeledi iliyotumiwa na askari tawala ni hatari.
2. Unga uliomwagika ulichafuka.
3. Magonjwa hayo yameenea mno.
4. Waganga ni waongo sana.
5. Nyua za maboma yao zinaporomoka.

## II. Zoezi la ziada

Andika kisa kuhusu shughuli iliyowahusisha watu wa ukoo wako kwa pamoja.

SURA YA 2

# SHULE YETU

Mada Ndogo ya 1:

## Kusikiliza na kuzungumza


### Shule yetu

Shuleni ni mahali ambapo panaendeleza shughuli za kufunza, kusoma na kuandika.

**Katika makundi ya wanne wanne, jadilinianeni michoro ifuatayo.**

1




| | | |
|---|---|---|
| 2  | 3  | 4   |
| 5  | 6  | 7  |

| | |
|---|---|
| 8.  | 9.  |
| 10.  | 11.  |

## Shairi

**Soma shairi lifuatalo kwa sauti kisha ujibu maswali.**

Kijana nenda usome, masomo yako shuleni,
Kuchezacheza ukome, siri imo vitabuni,
Kwa imara usimame, uvivuni kitu duni,
Kijana nenda usome, elimu ndiyo maisha.

Maisha leo magumu, usiposoma hatari,
Hupati vitu muhimu, nguo mlo, na sukari,
Kwanza uwe na elimu, ndipo uwe mashuhuri,
Kijana nenda usome, elimu ndiyo maisha..

Mahitaji sasa mengi, bila pesa huyapati,
Maisha bila msingi, hulivai hata shati,
Soma uwe serahangi, mtaalamu mtafiti,
Kijana nenda usome, elimu ndiyo maisha..

Maisha kama sunami, ni tufani yenye nguvu,
Bila akili kichwani, utaitwa mpumbavu,
Usome sana shuleni, usikubali uvivu,
Kijana nenda usome, elimu ndiyo maisha.


### Maswali

1. Katika ubeti wa kwanza mshairi anasema masomo yako wapi?
2. Taja vitu vitatu ambavyo mtu atakosa asiposoma kulingana na ubeti wa pili.
3. Kulingana na ubeti wa tatu mtu akisoma anaweza kufanya kazi gani?
4. Taja ujumbe unaojitokeza katika shairi hili.
5. Andika ubeti wanne katika lugha ya nathari.

## Mada Ndogo ya 2: Kusoma

**Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali.**

**Shuleni**



Ilikuwa siku ya furaha na shangwe shuleni mwetu kwani tulikuwa tumefika kipindi cha somo la Kiswahili. Punde mwalimu aliingia darasani na kutusalimia, “Hamjambo wanafunzi?” nasi tukamjibu, “Hatujambo mwalimu!” Mwalimu alitujulisha kuwa ulikuwa ni wakati wa somo la Kiswahili.Wanafunzi wote walitoa vitabu vyao vya kusoma na kuandikia. Mwalimu alitufunza na baadaye kutuuliza maswali.

Sikuelewa baadhi ya maswali. Kwa hivyo, niliinua mkono na kusema, “Tafadhali mwalimu,unaweza kunisaidia kujibu maswali haya?” Mwalimu hakusita ila alikuja mara moja na kuniongoza kutatua maswali. Kipindi cha Kiswahili kilipoisha mwalimu alituaga kwaheri. Mwalimu alielekea majilisini kutangamana na walimu wenzake siku hiyo. Mara sote tulikimbia nje kwa kipindi kifupi cha kupumzika.

Mwalimu Mkuu alionekana akitembea huku na kule kuhakikisha shughuli zote shuleni ziliendeshwa kwa utaratibu ufaao.Wavulana kwa wasichana walicheza michezo myepesi ya kuruka, kukimbia na hata mchezo wa kujificha. Mwalimu aliyeshughulika na maslahi ya wanafunzi alisimama kando na tulipokuwa tunachezea ili kuhakikisha usalama wa kila mmoja. Mara tulisikia ukemi kutoka upande mmoja wa uwanja. Mara mwalimu huyo alifika hapo kuchunguza kilichokuwa kimejiri. Mwalimu alipata ni mwanafunzi mmoja aliyemkanyaga mwenzake mguu kimakosa wakicheza.

Mwalimu alimsugua muathiriwa mguu kwa dawa. Mwanafunzi aliyemkanyanga mwenzake alimwomba msamaha. Shuleni mwetu mwanafunzi anapomkosea mwenzake humwomba msamaha kwa kumwambiia, “Pole! Nisamehe!” Naye mwathiriwa hujibu, “Nimepoa! Nimekusamehe!”

## Maswali

1. Andika msamiati wa shuleni uliotajwa katika kifungu hiki.
2. Taja salamu na mwitikio wa darasani kulingana na kifungu.
3. Mwalimu alipoingia darasani wanafunzi walitoa nini?
4. Taja maneno yanayoonyesha kuwa wanafunzi wamefunzwa msamiati wa adabu.
5. Ni nani huhakikisha shughuli za shuleni huendeshwa ifaavyo?

## Jibu maswali haya.

1. Chumba cha kusomea ni_________.
2. Anayefunza huitwa ______________.
3. _____________ni yule anayefunzwa.
4. Nakala ambayo mwanafunzi huandikia zoezi ni _________.

**Mada Ndogo ya 3:** **Sarufi**

## 1. Umoja na wingi wa nomino

**Nomino** ni jina la mtajo. Nomino hutaja mtu, kitu, ndege, mnyama, mahali na hali.Mifano ya nomino ni **mwalimu, shule, darasa, mkulima, mto, sufuria, jiwe, mnyama** na **ndege**.
Nomino huwa katika umoja na wingi.

**Kwa mfano:**

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| mwalimu | walimu |
| mtoto | watoto |
| mwanafunzi | wanafunzi |
| shule | shule |

### Zoezi

**a) Andika umoja na wingi wa nomino hizi.**

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| 1. mwalimu | __________ |
| 2. __________ | wanafunzi |
| 3. bendera | __________ |
| 4. __________ | kalamu |

5. mwalimu mkuu ___________
6. ____________ mazingira
7. wembe ___________
8. bawabu ___________
9. ua ___________
10. ___________ sekritari

**b) Andika sentensi katika wingi.**

1. Mwalimu alikuja.
2. Mwalimu mkuu anatufunza.
3. Kitabu kilisahihishwa.
4. Somo lilifunzwa vizuri.
5. Kalamu ilipotea.

## 2. Uakifishaji

Uakifishaji ni alama zinazotumika katika kuandika ili muktadha ueleweke. Alama hizi ni kama vile:

a) **Alama ya kiulizi(?)**-hutumika mwishoni mwa Sentensi ambayo ni swali. Kwa mfano:
Mwalimu amefika**? (kiulizi)**

b) **Alama ya koma (,)**-hutumika kuonyesha msomaji apumue.
Mfano: Mwanafunzi alibeba kalamu**,** wino**,** saa na raba.

c) **Alama ya kitone** (**.**) -hutumika mwishoni mwa sentensi na mkato wa maneno. Mfano:
i. Kitabu changu kimepotea**.**
**ii. Bw.** Muhidin Faruoq ndiye mwalimu mkuu.

**d) Herufi kubwa (H)** – hutumiwa mwanzoni mwa: sentensi, nomino ya pekee/halisi, mshororo wa shairi na kichwa cha kitabu. Kwa mfano:

i. Ninaenda shuleni kumwona mwalimu.
ii. Ukitaka kusherehekea, **Jumamosi** itakuwa siku nzuri kwako.
iii. **Suleimani** na **Rahabu** wataenda **Juba** kesho asubuhi.

**e) Herufi za mlazo** – hutumika kudhihirisha kichwa cha habari, jina lisilo la lugha inayorejelewa au neno lililotoholewa. Kwa mfano:

i. Kitabu *Shamba la wanyama* kinafunza mambo mengi.
ii. Siku hizi vijana wanapenda *watsap.*
ii. *Tamayya* ni chakula kitamu sana.

**f) Koloni (:)** – hutumika kuonyesha ujumbe unaofuata ni maelezo ya ziada, ujumbe wa ziada.

**g) Nusu koloni (;)** – hutumika: kuunganisha sentensi mbili zinazohusiana, kutenga maelezo na kinachoelezewa na mwisho wa mshororo wa shairi. Kwa mfano:

i. Bura; mkeka mkuukuu, siubadili na rehani; mkeka mpya.
ii. Nampenda kaka yangu; sima ndicho chakula chake.

**h) Mabano ()**– hutumika kufungia ujumbe wa ziada au maelezo. Kwa mfano: Mkombozi (mwanaharakati wa kutetea haki za watoto wa kiume) amechaguliwa kuwa mbunge.

**i) Ritifaa/king'ong'o(') –** hutumika kudhihirisha sauti ambayo ni king'ong'o na kuonyesha sauti imedondoshwa hasa katika ushairi. Kwa mfano:

i. Ng'ombe na kondoo ni ngeli ya A-WA.
ii. Wan'penda Amani yetu, wazalendo makinike,

**j) Mstari (________________)** – hutumika kupigia maneno au kichwa cha insha.

**k) Kistari kifupi (-)** – hutumika kutenganisha silabi au kudhihirisha nomino ambata. Kwa mfano:

i. Neno baba lina silabi mbili: ba-ba.

ii. Bata ni wengi: kuna bata-bukini, bata-mzinga, bata-kotwe na bata-maji

**l) Kihisishi/kiingizi (!)** – hutumika kudhihirisha hisia mbalimbali kama, furaha, huzuni, upendo, mshangao, uchungu. Kwa mfano:

i. Alhamdulillahi! Nimekupata ofisini.

ii. Yarabi! Umepoteza simu tena!

**m)** Dukuduku (…) – hutumika kudhihirisha usemi uliokatizwa, Kwa mfano:

**Lodu:** Hujambo Wani? Nilikusihi uwasilishe orodha ya wanariadha kwa mwali.

**Wani:** Sijambo Lodu! Nilifanya hivyo ila ….

**Lodu:** Ila akaikataa kwa vile ulipendelea darasa lako.

**Wani:** La hasha, alisema twende uwanjani leo jioni achague mwenyewe.

**n) Alama za mtajo/kunukuu (“ ”)** – hutumika kudhihirisha usemi halisi. Kwa mfano:

“Mbona tunapeperusha bendera Kila Jumatatu na Ijumaa shuleni?” Mkota aliuliza mwalimu

“Bendera ni ishara ya umoja, uhuru na amani. Tulipigania uhuru tulionao na tunaipeperusha ili kujikumbusha nchi yetu ni huru,” mwalimu alieleza.

## Zoezi

### a) Akifisha sentensi kwa kuweka alama iliyofungiwa.

**Mfano:**Ubao ulifutwa**(Swali) -** Ubao ulifutwa**?**

1. Mwanafunzi aliingia darasani (**swali)**
2. Mwalimu alisoma maswali majibu na kuyaandika. (**koma**)
3. Bendera ya shule ilipeperushwa (**swali**)
4. Kitabu cha Kiswahili kinasomwa (**kituo**)
5. Darasa viti na meza zimepaguswa. (**koma**)

### b) Akifisha aya ifuatayo.

heshima ni kitu cha maana mno wazee kwa vijana wavulana kwa wasichana wanafunzi kwa walimu sote ni binadamu iwe uko shuleni ama nyumbani ni vyema kuishi na kushirikiana na wenzako vyema hili hutokana na heshima ambayo huleta amani na utangamano kwa jamii isiyo na heshima miongoni mwa watu wake huwa haina ushirikiano mwema.

## Mada Ndogo ya 4: Kuandika

## Silabi za Kiswahili

Silabi ni sehemu ya neno inayojisimamia kisauti, mfano **a, ba, cha, nga, sa** na kadhalika. Silabi huunda neno. Kwa mfano:
a+ m +ka=amka,   m+ to+ to=mtoto.

### Aina za silabi za Kiswahili

1. Irabu
   Kuna silabi za irabu pekee. Kwa mfano:
   o-a = oa, u-a = ua, a-u = au

2. Konsonanti huru
   Kuna silabi za konsonanti huru. Kwa mfano:
   **m**-toto, mwana-**n**-chi, za

3. Konsonanti na irabu
   Kuna silabi za konsonanti na irabu. Kwa mfano:
   ka-ta- = kata, da-wa-ti = dawati, pi-la-u = pilau

4. Konsonanti, konsonanti na irabu
   Kuna silabi za konsonanti mbili na irabu. Kwa mfano:
   cha-i =chai, che-lewa = chelewa, mba-lamwezi = mbalamwezi

5. Konsonanti mbili na irabu
   Kuna silabi za konsonanti mbili, nusu irabu na irabu. Kwa mfano:

mbwe-ha = mbweha, ngwe-na = ngwena, mbwe-mbwe= mbwembwe

6. Konsonanti, nusu irabu na irabu
   Kuna silabi za konsonanti, nusu irabu na irabu. Kwa mfano: Mbala-mwe-zi = mbalamwezi, mwa-nga = mwanga, pwe-za = pweza

## Zoezi

**a) Tamka silabi hizi.**

a, ba, cha, da, dha, e, fa, ga, ha, i, ja, ka, la, ma, na, nga, nya, o, pa, ra, sa, sha, ta, tha, u, va, wa, ya, za.

**b) Mkiwa kwa makundi ya wawili wawili, tamkeni kwa sauti silabi hizi.**

1. ra, la
2. sa, sha
3. cha, za
4. ja, ya
5. ba, pa, va
6. na, nya
7. ka, ga
8. da, dha
9. ya, wa
10. a, e

**c) Tunga maneno kumi ukitumia silabi za swali (b), hapo juu.**


## Mada Ndogo ya 5: Msamiati

**Maumbo**

Maumbo ni neno linalotokana na umbo, kwa hali ya umoja. Ni mkao wa kitu, Kilivyoundwa, au kilivyoumbwa.

**Aina za maumbo:**


1.



Hii ni duara

Duara ni aina ya mviringo

2.



Huu ni mraba.


Una pande nne zilizo sawa.

3.




Huu ni mstatili.
Sambamba ni sawa

.4.




Pembetatu.

5




Duara dufu.

6.




Nyota.

7.



Almasi.

8.



Moyo.

9.




Pembenane

10.




Tenge

11.




Pembetano

12.



Pembesita

13.



Msalaba

**Zoezi**

a. Mkiwa kwa makundi ya wawili wawili, jadilianeni maumbo na rangi katika michori.
b. Wewe na mwenzako, peaneni orotha ya vitu vingine vilivyo na maumbo na ranzi mlizopewa.
c. Mkiwa kwa makundi ya wanne wanne, endeni sokoni, na muandike orotha ya vyakula vilivyo na rangi na maumbo mlioyasoma.

# SURA YA 3

# UCHUKUZI


## Mada Ndogo ya 1: Kusikiliza na kuzungumza

### Uchukuzi

### Zoezi

**a) Andika majina ya vyombo hivi vya usafiri.**

| | |
|---|---|
| 1.  | 2.  |

| | |
|---|---|
| 3.  | 4.  |
| 5.  | 6.  |
| 7.  | |
| 8.  | |

| | |
|---|---|
| 9.  | 10.  |

**Tamka maneno yafuatayo.**

1. uchukuzi
2. matatu
3. baiskeli
4. pikipiki
5. gari
6. lori
7. ndege
8. meli

## Shairi

**Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

Hodi hodi ninabisha, kwa wenzangu majirani,
**S**alamu nazifikisha, kwa kilio cha undani,
Ujumbe nawasilisha, wanaoenda safarini,

Utulinde Maulana, tuwe mbali na hatari.
Ajali kinga haina, huwezi kuitabiri,
Hutokea kiaina, kwa vyombo vya usafiri,
Iwe meli na matwana, magari mpaka na feri,
Utulinde Maulana, tuwe mbali na hatari.

Natishwa si masihara, kukicha mi nafikiri,
Tusimameni imara, kuepuka yasijiri,
Yasitoke kila mara, kwa vyombo vya usafiri,
Tusijepata hasara, na ajali kukithiri.

Tuzingatie sheria, zilotunga taasisi,
Ujumbe kwa abiria, epukani na mikosi,
Usipende kudandia, ukiikosa nafasi,
Mja wakusubiria, sitara huwa hakosi.
Manahodha na marubani, madereva mjuao,
Mkijaza na pomoni, siongeze mubebao,
Kining'inia langoni, mpo hatarini nao,
Sijifanye hamuoni, lawama kwenu na kwao.

Tazameni usalama, ombi langu lisikike,
Kondakta twaama, masikio mupulike,
Vyombo visije kwama, tusafiripo tufike,
Tushikamane daima, jamani tuwajibike.

## Zoezi

1. Mshairi anaomba nini katika ubeti wa kwanza?
2. Kulingana na ubeti wa pili taja vyombo vinne vya usafiri vinavyoweza kupata ajali.
3. Mshairi anawaomba kina nani wadumishe usalama katika uchukuzi katika ubeti wa 5 na 6?

## Mada Ndogo ya 2: Kusoma

**Someni kifungu hiki kwa sauti katika vikundi kisha mjibu maswali.**

### USAFIRI

Usafiri ni shughuli za kupeleka au kusafirisha watu au mizigo, kutoka mahali moja hadi mahali pengine. Katika kusafiri na kusafirisha vitu, mwanadamu anaweza kutumia aina nyingi za usafiri. Anaweza kupitia ardhini au nchi kavu, kupitia majini na kupitia angani. Wakati mwingine, watu hutembea. Mtu anayesafiri kutumia vyombo vya usafiri anaitwa abiria. Abiria anapaswa kulipa ada ya kusafiri iitwayo nauli.

Katika kusafiri katika nchi kavu, wanadamu hutumia matwana, basi, pikipiki, motokaa na garimoshi.

Kwa kusafirisha mizigo au shehena kubwa, watu hutumia mikokoteni, lori na mabogi. Pia kuna wanaotumia wanyama kama punda, ngamia, ng’ombe na farasi.




Majini vyombo vya usafiri ni kama meli, jahazi, ngalawa, dau, na mashua. Ndege ndio hutumika sana angani. Ndege husafiri kwa mwendo wa kasi sana. Mataifa mengi hutumia usafiri wa ndege kwa sababu ni wa haraka. Ndege husafirisha wanadamu na shehena ya vitu vinvyotakikana haraka au vitu vinvoweza kuharibika haraka vikiwekwa muda mrefu.

## Maswali

1. Elezea vyombo vya usafiri vilivyotajwa katika taarifa.
2. Elezea basi chombo kimoja kati ya vile vilivyotajwa jinsi kinavyo tumika.

## Mada Ndogo ya 3:

## Sarufi

**Zoezi**

**a) Chagua jibu sahihi kutoka kwa majibu yaliyofungiwa.**

1. Chombo cha usafiri kinachopitia majini ni ______. (meli,gari)
2. ________ni Kubebwa na chombo cha uchukuzi.(kusafiri,kukimbia)
3. _________ ni chombo kikubwa sana cha uchukuzi.(baiskeli,ndege)
4. Mtu anayeendesha gari huitwa_________.(abiria,dereva)
5. Malipo anayolipa mtu anaposafiri ni _______. (nauli, abiria)

**b) Jaza nafasi kwa msamiati sahihi wa usafiri.**

Usafiri au ______ ni njia ambazo hutumika kwa kusafiria.Hutumia vyombo kama vile baiskeli_______,_______na _______.Kuna vyombo vya usafiri ambavyo hutumia barabara, kama vile _______,_______, gari na lori. Vingine husafiria hewani kama vile _______.Meli husafiria majini. Mtu anayesafiri huitwa msafiri au _______**.**Msafiri anapaswa kuulizia wakati au saaambazo chombo cha usafiri kitaondoka ili asiachwe. Pia aulize mwelekeo au kule ambako chombo hicho kinaenda ili asipotee. Mtu anapoabiri chombo cha usafiri analipa kondakta pesa zinazoitwa _______**.**

## Mada Ndogo ya 4: Kuandika

**Zoezi**

1. Andika kisa juu ya safari uliosafiri.
2. Wewe na mwenzako andikeni kisa juu ya umuhimu wa vyombo vya uchukuzi.

## Mada Ndogo ya 5: Msamiati

### Nyakati na Saa

Wakati ni kipindi Fulani cha muda. Saa ni chombo ambacho hutuonyesha wakati. Siku nzima huwa na saa ishirini na nne,yaani saa kumi na mbili usiku kucha na saa kumi na mbili mchana kutwa.

Kipindi cha saa moja huwa na dakika sitini . Nusu saa ni sawa na dakika thelathini. Robo saa ni sawa na dakika kumi na tano. Dakika moja nayo huwa na sekunde sitini. Sekunde pia huitwa nukta.

**Mchoro wa saa**

Usomaji wa saa kwa Kiswahili

Angalieni mchoro huu wa saa, kisha mjadiliane kwa makundi.




Iwapo saa imeandikwa kwa tarakimu, tutaisoma tarakimu ile vile tunavyosoma uso wa saa.

**Iangalie mifano ifuatayo kwa makini.**

Saa 7.15 -Saa saba na dakika kumi na tano au saa saba na robo wala si saa moja na robo.

Saa 10.30 -Saa kumi na nusu, au saa kumi unusu au saa kumi na dakika thelathini.

Saa 4.30 -Saa nne unusu.

Saa 1.15 -Saa moja na dakika kumi na tano au saa moja na robo.

Saa 9.45 -Saa tisa na dakika arobaini na tano au saa kumi kasorobo.

Iwapo zimepita dakika thelathini, badala ya kusema dakika thelathini, unaweza kusema nusu. k.m. Saa 12.30 – unaweza kusema saa kumi na mbili unusu au saa kumina mbili na nusu.

Iwapo zimepita dakika kumi na tano, unaweza tumia robo badala ya dakika kumi na tano. k.m.
Saa 2.15 – saa mbili na dakika kumi na tano au saa mbili na robo.
Iwapo zimepita dakika arobaini na tano, unastahili kutumia kasoro robo au kasorobo. k.m. Saa 6.45 – saa saba kasorobo. Maana yake ni kuwa, bado dakika kumi na tano (robo saa) itimie saa saba.

## Siku za Juma

Juma au wiki moja huwa na siku saba. Yafuatayo ni majina ya siku za juma.

| **Siku za wiki** |
|---|
| Jumapili siku ya kwanza ya wiki. |
| Jumatatu siku ya pili ya wiki. |
| Jumanne siku ya tatu ya wiki. |
| Jumatano siku ya nne ya wiki. |
| Alhamisi siku ya tano ya wiki. |
| Ijumaa siku ya sita ya wiki. |
| Jumamosi siku ya saba ya wiki. |

**Siku Zikilinganishwa na Leo**

**Haya ni majina tunayotumia kurejelea siku zinazokaribiana na leo.**

| SIKU | MAELEZO | MFANO |
|---|---|---|
| juzi | siku iliyotangulia jana | ikiwa leo ni Jumatano, juzi ilikuwa Jumatatu. |
| jana | siku iliyotangulia leo | ikiwa leo ni Jumatano, jana ilikuwa Jumanne. |
| leo | siku ambayo tuko sasa hivi | |
| kesho | siku inayofuata leo. | Ikiwa leo ni Jumatano, kesho itakuwa Alhamisi. |
| kesho kutwa | siku itakayokuja baada ya kesho. | ikiwa leo ni Jumatano, kesho kutwa itakuwa jumaa. |
| mtondo goo | siku itakayokuja baada ya kesho, ni kesho kutwa. siku tatu kutoka leo | ikiwa leo ni Jumatano, kesho kutwa itakuwa Jumamosi. |

## Miezi ya Mwaka

**Jedwali lifuatalo linaonyesha majina ya miezi katika mwaka, na idadi ya siku katika kila mwezi.**

| | JINA | MWEZI WA: | SIKU |
|---|---|---|---|
| 1 | Januari | kwanza | 31 |
| 2 | Februari | pili | 28 |
| 3 | Machi | tatu | 31 |
| 4 | Aprili | nne | 30 |
| 5 | Mei | tano | 31 |
| 6 | Juni | sita | 30 |
| 7 | Julai | saba | 31 |
| 8 | Agosti | nane | 31 |
| 9 | Septemba | tisa | 30 |
| 10 | Oktoba | kumi | 31 |
| 11 | Novemba | kumi na moja | 30 |
| 12 | Desemba | kumi na mbili | 31 |

## Zoezi

1. Mkiwa kwa makundi ya wawili wawili, jadilianeni siku na miezi yenu yakuzaliwa.
2. Andika orodha siku unzoenda shuleni.

## Masaa ya Siku

Yafuatayo ni mafungu ya masaa au nyakati mbalimbali za siku.

| WAKATI | MAELEZO | MASAA |
|---|---|---|
| mchana | wakati wa siku wenye jua. kutoka saa kumi na mbili asubuhi hadi saa moja jioni hivi. | 6am - 7pm |
| usiku | wakati wa siku usiokuwa na jua. kutoka saa moja jioni hadi saa kumi na mbili siku inayofuatia. | 7pm - 6am |
| alfajiri | kati ya saa tisa na saa kumi na moja asubuhi. | 3am - 5am |
| macheo | saa kumi na moja hadi saa kumi na mbili hivi jua linapochomoza. | 3am - 5am |
| asubuhi | kutoka saa kumi na mbili hadi saa sita za mchana. | 6am - 12pm |
| adhuhuri | saa sita za mchana hadi saa nane. | 12pm - 2pm |
| alasiri | saa nane hadi saa kumi na moja hivi. | 2pm - 5pm |
| jioni | saa kumi na moja hadi saa moja jioni. | 5pm - 6pm |
| machweo/ magharibi | saa kumi na mbili hadi saa moja jioni; jua linapotua. | 6pm - 7pm |
| usiku mchanga | kati ya saa moja jioni na saa sita za usiku. | 7pm - 12am |
| usiku wa manane | kutoka saa sita za usiku hadi alfajiri. | 12am - 3am |

## Umbali

Umbali ni maelezo ya urefu wa kimasafa baina ya vitu viwili tofauti.

Umbali unaweza kutaja urefu wa kimwili au kukadiria kuzingatia vigezo vingine. Katika hisabati umbali kazi au tani ni dhana ya umbali wa kimwili.


# SURA YA 4

# MWILI NA USAFI

## Mada Ndogo ya 1:

## Kusoma

## A: Sehemu hizi za mwili.



## Zoezi: Una ngapi?











**Zoezi: Ambatanisha sehemu ya mwili na kazi yake.**

kuona

kutembea

kukula

kusikia

kugusa

kunusa













## Mada Ndogo ya 2: Kusikiliza na kuzungumza

### Shairi

**Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

**AFYA YAKO**

Afya ukijaliwa, hilo ni deni tambua,
Yafaa kuitumia, kwa yale yatayokufaa,
Siku zikishatimia, thawabu kujivunia,
Afya yako ni deni!

Naam utashangaa, haya ukiyasikia,
Bali nakuhakikishia, ni ukweli ulotimia,
Kama hukuyajua, macho nimekufungua,
Afya yako ni deni!

Askari hudaiwa, na wao pia raia,
Ole wao watumiwa, na hawatasaidiwa,
Kila wakisingizia, kidole kwa hurejea,
Afya yako ni deni!

Nguvu waliotumia, wanafunzi kuwavaa,
Au wapole raia, waliojikutania,
Na maandamano yakawa, salama yenye ulua,
Afya yako ni deni!

Nesi wanaowaua, wagonjwa huku wajua,
Nao watasimulia, huku ukiwa wakiwa,
Wasiamini kujua, wenye aya wayajua,
Afya yako ni deni!

Madaktari nao pia, kitabu kitasogea,
Ukweli kuugundua, sivyo walivyoamua,
Nafsi kutangulia, Muumba hakukusudia,
Afya yako ni deni!

Wanasiasa wakiwa, zamu itawafikiya,
Midomo itanyamaa, la kujibu kutojua,
Midomo itaamua, yenyewe kujisemea,
Afya yako ni deni!

## Maswali

1. Taja watu watatu ambao watadaiwa kwa sababu ya afya.
2. Kwa nini mshairi anawalaumu manesi?
3. Eleza ujumbe wa shairi hili.

## Mada Ndogo ya 3: Kusoma

**Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali.**

### MWILI NA USAFI

Mwili huhitaji kupumzishwa na pia kufanyishwa mazoezi. Mazoezi ya mwili husaidia kuondoa uchovu na kusafirisha damu mishipani kwa wepesi. Mtu akikosa kufanya mazoezi anapatwa na uchovu usio wa kawaida, ananenepa nakuhatarisha maisha yake. Mwili unahitaji kupumzishwa kwa kulala, kuoshwa na kupewa vyakula vyenye afya, yakiwemo matunda na mboga za kila aina. Mtu anapooga anaondoa jasho na uchafu mwilini ujulikanao kama **kizimwili.** Watu wachafu hujawa na **nta** masikioni na **matongo** machoni kwa sababu yakutoosha uso. Wakifungua vinywa vyao karibu na wewe utatoroka, vinywa hunuka fee, utadhani samaki wameozeana ndani!



Nguo anazovaa mtu zinahitaji kuoshwa na kuanikwa zikauke.Mtu akikosa kuosha na kubadilisha nguo, anatoa harufu mbaya isiyopendeza. Baadhi ya watu hawa wachafu hawaoshi mavazi yao sana sana nguo za ndani au chupi. Jameni maisha gani haya! Hata wanyama kwa njia mbalimbali husafisha mili yao. Kwa mfano, utamuona paka mama akilambalamba kitoto chake

ngozi kukiondoa uchafu. Je, binadamu tunashindwa usafi na wanyama wasio na akili kama sisi?

Uchafu wa mwili humfanya mtu avamiwe na wadudu kama chawa. Pia anaweza kupatwa na magonjwa ya ngozi. Mwili unapaswa kuoshwa kwa sabuni, kitambaa cha kuoga na maji safi. Baadhi ya watu huogea na kuoshea kwenye vijito. Tabia kama hii si nzuri kwa usafi na afya ya mtu kwa sababu huenda mtu akaambukizwa magonjwa. Pia uchafu wanaomwaga katika vijito humo huenda ukawadhuru watu wanaoyatumia maji haya kuyanywa bila kuchemsha. Usafi wa mwili ni pamoja na kukata kucha za vidole, kuchana nywele, kupiga mswaki na kuvaa nguo safi. Mazoezi ya mwili pia husaidia mtu kuwa na afya.

## Maswali

1. Taja njia mbili za kuupumzisha mwili.
2. Kulingana na kifungu,taja madhara matatu yanayomkumba mtu asiyeoga.
3. Taja aina zozote tano za usafi.
4. Eleza maana ya msamiti huukama ulivyotumika katika kifungu.

   i) nta    ii) matongo

## Mada Ndogo ya 4: Sarufi

### Maneno yenye sauti zinazorudiwa

Lugha ya Kiswahili ina maneno yenye silabi zinazorudiwa.

Kwa mfano:

ba+ba=baba, cha+cha=chacha

### Zoezi

**a) Tunga sentensi ukitumia maneno haya.**

1. usafi
2. kupiga mswaki
3. maji safi
4. choo safi
5. kuosha nguo

**b) Andika silabi hizi kwa kurudia ili kuunda neno.**

Kwa mfano: la - lala

1. po
2. ka
3. ba
4. nya
5. go
6. ya
7. cha
8. lu
9. tinga
10. piki

**c) Jaza sentensi hizi kwa sauti ya kurudiaruarudia.**

1. Dereva anaendesha tinga________.
2. Meno yake yanameta________.
3. Mtoto anakula pi____.
4. Pa____ anaishi baharini.
5. Nilimtembelea nya_____.

## Mada Ndogo ya 5: Kuandika

1. Andika vifaa vya lazima ambavyo mtu anapaswa kutumia kwa kuoga.
2. Wewe pamoja na mwenzako, andikeni kisa kitakachoishia, “Tangu siku hiyo nilitambua umuhimu wa usafi wa mwili”.

# SURA YA 5

# NYUMBANI KWETU

## Mada Ndogo ya 1:

## Kusikiliza na kuzungumza



# Shairi

## Soma shairi hilikisha ujibu maswali.

Makaazi ni nyumba,
Imejengwa kwa matofali,
Kwa boriti, kwa kuta
Na vingi vijiti.

Makaazi ni nyumba,
Waishipo watu,
Salama huekwa,
Kwa joto na starehe ndani.

Makaazi ni nyumba,
Waliapo familia,
Meza wakizunguka,
Wakati wa mlo.

Makaazi ni nyumba,
Kazi ya kinyumba yafanyika,
Kufagia, kuosha na kupanga,
Kusafisha mazingira.

Makaazi ni nyumba,
Waishipo watu,
Familia inayonipenda,
Na inasimama kando yangu.


Makaazi ni nyumba,
Upendo na adabu hukuzwa,
Lakini bado ni makaazi,
Nyumbani ni nyumbani.

## Maswali

1. Mshairi anatoa sifa gani za nyumba katika ubeti wa kwanza?
2. Ni shughuli zipi zinazofanywa nyumbani?
3. Taja mambo mawili yanayokuzwa nyumbani.
4. Eleza ni kwa nini nyumbani ni nyumbani.

## A. Tazama picha zifuatazo.

**Jadiliana na mwenzako kuhusu shughuli za nyumbani zinazoendelezwa.**

| | |
|---|---|
| 1.  | 2.  |
| 3.  | 4.  |
| 5.  | 6.  |

## Mada Ndogo ya 2: Kusoma

## Mazungumzo: Marafiki wawili

**Wewe na mwenzako someni mazungumzo haya.**

| | |
|---|---|
| AYEN: | Hujambo ohide.Habari ya leo? |
| OHIDE: | Sijambo Ayen.**Sina** neno. |
| AYEN: | Je,Ohide, nyumbanini wapi? |
| OHIDE: | Nyumbani kwetu ni Mashariki.Wazazi wangu wamejenga nyumba huko.Sisi **hatuishi** mjini. |
| AYEN: | Ah!Vizuri sana.Nyumba yenu ina vyumba vingapi? |
| OHIDE: | Nyumba yetu ina vyumba vinne.Chumba kimoja ni cha maakuli,kingine ambacho **si** kikubwa sana ni jikoni.Vile vingine viwili ni vya kulala. |
| AYEN: | Chumba cha maakuli ni kipi? |
| OHIDE: | Hiki ni kile ambacho watu hukaa wakipumzika na pia hutumika wakati wa kula.Chumba hiki kimewekwa viti,meza,redio na hata televisheni.Chumba hiki **hakiwekwi** vitu vingi sana. |
| AYEN: | Ho!Na kile cha kupikia? |
| OHIDE: | Chumba hiki ndicho cha kupikia.Kina vyombo vyote vya upishi kama vile jiko,sufuria na miko, sahani, vijiko,bakuli na vingine pia huwekwa hapa. |
| AYEN: | Wewe unapokuwa nyumbani hufanya kazi za nyumbani? |

OHIDE Ndio, mimi hufanya kazi za nyumbani. Mimi **sikai** bure nyumbani.Hufagia chumba na kuosha vyombo.Kakangu hunisaidia kufyeka nyasi na kuchoma taka.Wazazi wetu hutuhimiza tufanye kazi,**hawapendi** tukiwa wavivu.

AYEN: Ni kweli Boi.Mtoto **asiyesaidia** kazi za nyumba ni mvivu.

## Maswali

1. Katika kifungu hiki kwa kina Ayen ni wapi?
2. Taja idadi ya vyumba katika nyumba ya kina Ayen.
3. Chumba cha maakuli hutumika vipi?

## Zoezi.1Andika majina ya vyombo na vifaa vya nyumbani vifuatavyo.

| 1. | 2. |
|---|---|
|  |  |

| | |
|---|---|
| 3.  | 4.  |
| 5.  | 6.  |

## Zoezi 2: Chora picha ya Televisheni na redio.

## Mada Ndogo ya 3: Sarufi

### Ukanushaji wa kitenzi

**Kitenzi ni kitendo** kwa mfano,lia,kula,kimbia,keti,soma,vaa na kadhalika.Vitenzi vya Kiswahili vinakanushwa kwa kutumia **si** au **ha**.Kwa mfano:

| KITENZI | UKANUSHO WA KITENZI |
|---|---|
| 1. Anakula. | Hali. |
| 2. Aliimba. | Hakuimba. |
| 3. Watacheza. | Hawatacheza. |
| 4. Analia. | Halii. |

### Nyakati

Huonyesha wakati wa kitendo; inaweza kuwa kitendo kilichukua, kinachukua, kitachukua, kimechukua au huchukua nafasi kwa wakati uliotajwa katika kitenzi. Lugha ya Kiswahili hutumia nyakati mbalimbali. Kwa mfano:

Wakati uliopita - hutumia **LI.**Kwa mfano: Mtoto **aliwalisha** kuku.
Wakati uliopo -hutumia **NA.** Kwa mfano: Bibi **anafagia** barazani.
Wakati ujao- hutumia **TA.** Kwa mfano: Dereva **ataosha** pikipiki.
Hali isiyodhihirika-hutumia **A.** Kwa mfano: Zuhura an**afagia** chumba**.**
Hali ya mazoea -hutumia **HU.** Kwa mfano: Mama **hupika.**

Hali timilifu – hutumia **ME**. Kwa mfano: Mgeni **amefika**.

## Kukanusha

Kukanusha ni kukataa. Tunapokanusha huwa tunakataa kitendo hakikutendeka.

### Nyakati huwa na ukanusho wake.
### Kwa mfano:

| wakati | Kitenzi | Kitenzi pamoja na wakati | Ukanusho |
|---|---|---|---|
| Wakati uliopita | cheza | A**li**cheza. | **Ha**kucheza. |
| Wakati uliopo | cheza | A**na**cheza. | **Ha**chezi. |
| Wakati ujao | cheza | A**ta**cheza. | **Ha**tacheza. |
| Hali isiyodhihirika | cheza | **A**cheza. | **Ha**chezi. |
| Hali ya mazoea | cheza | **Hu**cheza. | Huwa **ha**chezi. |
| Hali timilifu | cheza | A**me**cheza | Ha**ja**cheza. |

## Zoezi

### a) Andika wakati uliotumika katika sentensi katika mabano.

Mfano: Nitaenda dukani. (Wakati ujao)

1. Yaya amemlaza mtoto. (___________)
2. Nchi yetu inapendeza. (___________)

3. Jirani yao alifuga kuku. (__________)
4. Mito yote ilifurika. (__________)
5. Sinia zote zinaoshwa. (__________)
6. Ufagio mpya utanunuliwa. ( __________ )
7. Mama anamlaki mgeni. ( __________ )
8. Mwalimu anaingia darasani kila siku. ( __________ )
9. Watamkaribisha mwenzao leo. ( __________ )
10. Mlimtembelea babu yenu? ( __________ )

**b) Kanusha vitenzi katika sentensi hizi.**

1. Mama anapika chakula.
2. Mtamwimbia nyanya wimbo.
3. Kuku wetu alitaga mayai.
4. Natumia maji kuosha choo chetu.
5. Nyumba yetu inajengwa upya.
6. Mfanyakazi wao ataenda shambani.
7. Chumba cha kulala kina vitanda viwili.
8. Chakula cha kikwetu kinapendeza.
9. Watakunywa maziwa yote.
10. Tulichemshia maji ya kunywa jikoni.

## Mada Ndogo ya 4: Kuandika

### Kutunga sentensi

**Andika sentensi tano ukitumia ukanusho wa vitenzi.**

1. ________________________________________
2. ________________________________________
3. ________________________________________
4. ________________________________________
5. ________________________________________

## Mada Ndogo ya 4: Msamiati

### Mavazi

Mavazi huvaliwa kwa mwili ili kujifunika.

Aina ya mavazi:






Rinda shati tai Suruali ndefu





Kaptura sketi koti






Kofia soksi jaketi

# SURA YA 6

## USHIRIKIANO, AMANI NA UTULIVU

**Mada Ndogo ya 1:** **Kusikiliza na kuzungumza**

| 1. | 2. |
|---|---|
|  Wanakijiji wakishirikiana kuteka maji ya kunyunyuzia mimea. |  Wanakijiji wakishikiana katika upanzi wa mimea iletayo chakula. |

| | |
|---|---|
| 3.  Wanakijiji wakishirikiana kusafisha mazingira. | 4.  Deng anamwomba askari amsaidie kuvuka barabara yenye magari mengi. |

Ushirikiano,amani na utulivu ni wakati watu wanaoishi mahali fulani wanakaa kwa upendo, amani na umoja bila chuki au kubaguana. Msamiati unaohusiana na haya ni kama **umoja, upendo, kujali maslahi ya wengine, heshima na kusaidiana**.

## Zoezi

**Soma shairi hili kwa sauti kisha ujibu maswali.**

**UCHAGUZI WANUKIA**

Enyi ndugu wazalendo, nahubiria hadhara,
Tuzidi kukaza mwendo, kuongoza msafara,
Uongozi ni vitendo, si fujo wala papara,
Uchaguzi wanukia, nampa anotujali.

Napuliza vuvuzela, kusema kwa ukaidi,
Msinizuge kwa hela, kura yangu siinadi,
Viongozi mna hila, ondoeni itikadi,
Uchaguzi wanukia, nampa anotujali.

Mmezoea kusema, maneno yaso busara,
Hamna utu na wema, raia twagaragara,
Nia zenu sio njema, bungeni ni mishahara,
Uchaguzi wanukia, nampa anotujali.

Uongozi wa tamaa, ulobeba ubinafsi,
Mkatuwacha na njaa, kutudhulumu nafusi,
Katakata nakataa, nyoyo zenu ni nyeusi,
Uchaguzi wanukia, nampa anotujali.

Msidhani tuna chongo, twaona mnayofanya,
Tumefunguka mabongo, acheni kutudanganya,
Kura sipigi kwa hongo, komeni ninawakanya,
Uchaguzi wanukia, nampa anotujali.

*(Imenukuliwa kutoka kwa* HAMZA A. MOHAMMED)

## Maswali

1. Mshairi analalamikia nini katika ubeti wa tatu?
2. Mshairi anasema atampa kura yake nani?
3. Taja ujumbe wa shairi.

## Mada Ndogo ya 2: Kusoma

**Soma kisa kifuatacho kisha ujibu maswali.**

### USHIRIKIANO



Ushirikiano ni hali ya kujitolea na kuishi vyema na wengine. Ushirikiano huleta amani na utulivu.Kuipenda nchi si kwa maneno tu bali kwa vitendo. Muhimu zaidi ni wananchi kupendana na kushiriki katika miradi ambayo inaweza kuboresha maisha yao na kuwafurahisha.

Ushirikiano unaweza kuonyeshwa kupitia kwa kujitolea kwa mambo ya taifa lako kama vile michezo na usalama. Wananchi wanapaswa kushirikiana nakushangilia timu za nchi yao, lakini usistaajabu kuona wananchi wakishangilia timu za kigeni na hata wakati mwingine mashabiki wa timu pinzani wanaweza pigana. Wanawafahamu wachezaji wote wa timu hizo ilhali hata pengine

wengine wao hawatapata fursa ya kuonana nao maishani. Mashabiki hao hao waulize kuhusu timu za humu nchini na utashangaa hawana habari. Je, ushirikiano ulienda wapi?

Ushirikiano ni suluhisho la matatizo yote ya nchi. Miongoni mwetu kuna watoto mayatima wanaohitaji usaidizi;wazee wakongwe wanaohitaji angalau mtu wa kuwafaa;Sehemu nyingine za nchi zimekumbwa na ukame na njaa;mara kwa mara tunasikia uvamizi katika sehemu kadha wa kadha humu nchini.Haya yote yanaashiria ukosefu wa ushirikiano miongoni mwa wananchi.Mwananchi aliyejitolea kwa niaba ya mwenzake hatawaangalia wengine wakienda miayo kwa sababu ya njaa huku yeye akiteuka kwa kushiba!Ushirikiano utamfanya amfae anayeenda miayo kwa chakula hata kama ni kidogo.Watoto hawatakosa karo ya shule katika nchi iliyo na ushirikiano.

Watu wanapoishi pamoja,wanahitaji ushirikiano, haki, amanina utulivu.Watu wakishirikiana wanafanya mambo kwa pamoja.Amani ni kuishi bila vitisho,vita au hata chuki.Watu wakikosa amani hawana furaha kwa sababu ya visa kama vile kuwapiga wenzao kabari au kuwatapeli.

Amani huleta utulivu.Siku ambayo kila mtu atakuwa na amani na utulivu, tutaacha kufuga mbwa. Hatutaunda milango ya chuma wala nyumba zetu kuwa na silaha. Mtu akibisha mlango, tutafungua bila kuuliza ni nani. Tutatembea usiku bila kuangalia nyuma kwa kuogopa.Utulivu huwezesha watu kuendeleza shughuli zao bila woga.

Wanafunzi wakiwa na ushirikiano shuleni watasoma pamoja na kupita mitihani yao.Nchi ikiwa na amani itaweza kuendelea sana kiuchumi.Wananchi wake watafanya kazi zao bila woga na hivyo kuzalisha raslimali ya nchi.Kama nchi ina utulivu, watalii wataitembelea hivyo kuinua uchumi wa nchi.

Vyombo vya habari,majarida na magazeti yanapaswa kueneza matangazo na ujumbe wa ushirikiano,amani na utulivu.Waandishi wa vitabu na makala mbalimbali yashughulikie masuala ya ushirikiano,amani na utulivu.

## Maswali

1. Kulingana na kifungu ushirikiano ni nini?
2. Ni nini kinaudhi mwandishi juu ya mashabiki wa mpira?
3. Ushirikianao unawafaidije wanafunzi?
4. Jadili faida za amani katika makazi ya watu kulingana na kifungu.
5. Taja na ueleze njia zozote nne ambazo tunaweza kutumia vyombo vya habari kuleta utangamano miongoni mwa wananchi.

## Mada Ndogo ya 2: Sarufi

## Zoezi

**Tunga sentensi ukitumia manenoyafuatayo:**

1. amani
2. makubaliano
3. ushirikiano
4. vita
5. undugu

## Mada Ndogo ya 3: Kuandika

1. Soma gazeti na uandike ujumbe wa kitaifa unaojitokeza humo.
2. Kutoka kwa kamusi andika maana ya maneno yafuatayo:
   a) taifa
   b) mwananchi
   c) maridhiano